



CHUO KIKUU CHA TUMAINI MAKUMIRA
OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO TAALUMA
S.L.P 55, USA-RIVER, ARUSHA

TANGAZO LA MAHAFALI

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha, anayo furaha kuwatangazia wanafunzi wote wanaohitimu masomo yao kwa mwaka wa masomo 2016/2017 kwamba, **Mahafali ya 61 ya Chuo cha Kilutheri cha Theologia Makumira, Mahafali ya 21 MUCO, na Mahafali ya 7 kwa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira**, yatafanyika siku ya Jumamosi tarehe 2 Disemba 2017, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha, kuanzia saa 3:00 Asubuhi.

Tarehe za Mahafali

1. **Alhamisi:** Tarehe 30/11/2017
 - **Kuchukua majoho** (saa 3 asubuhi hadi saa 10 jioni)
2. **Ijumaa:** Tarehe 01/12/2017
 - **Jumuiko la Wahitimu - Convocation na mazoezi ya mahafali** (saa 3 asubuhi hadi saa 9 alasiri)
3. **Jumamosi:** Tarehe 02/12/2017
 - **Siku ya Mahafali (Graduation Day) –**
(saa 2:30 asubuhi hadi saa 8:00 mchana)

Masharti

1. Wahitimu wote mnahitajika kushiriki kwenye **Jumuiko la Wahitimu** (Convocation day) siku ya Ijumaa tarehe 01 Disemba 2017 kuanzia saa 3.00 Asubuhi mpaka saa 9 Alasiri ambapo mtapewa taratibu za mahafali
2. Wahitimu ambao hawatahudhuria jumuiko hilo, hawatarusiwa kushiriki katika mahafali.
3. Majoho lazima yarudishwe Jumatatu Tar 04 Disemba 2017, vinginevyo kutakuwa na faini ya shilingi 20,000/-.

WOTE MNAKARIBISHWA

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma